

**HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE WAKATI WA
KUZUNGUMZA NA WAKE WA VIONGOZI – NEW MILLENIUM
GROUP, DAR ES SALAAM - VIWANJA VYA WAMA TAREHE**

08 JULAI, 2010

Mwenyekiti wa Wake wa Viongozi , Mama Germina Lukuvi

Waheshimiwa Wajumbe wa Bodi ya WAMA,

Wake wa Viongozi,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana,

Habari za Mchana!

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutanika hapa leo. Nawashukuruni wote kwa kufika hapa leo na kwa zawadi zenu nzuri mlizonikabidhi. Asanteni sana!

Ndugu Wakinamama Wenzangu,

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwenu kwa kutambua mchango wangu na wa Taasisi yetu ya WAMA katika kuchangia maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

Taasisi yetu inatambua mchango mkubwa wa wakinamama katika kuleta Maendeleo ya nchi hii. Hivyo basi nasi tumekuwa mstari wa mbele katika kusaidia upatikanaji wa fursa za elimu, afya na maendeleo ya kiuchumi kwa wasichana na wakinamama. Pamoja na watoto yatima na wanaotoka katika mazingira magumu.

Kwangu mimi leo hii ni faraja kubwa kuona wanawake wanashirikiana kwa pamoja katika utekelezaji wa mambo makubwa muhimu. Nawasihi basi nayi wake wa viongozi muendeleze jitihada zenu za kumkomboa mwanamke na hatimaye kuleta mabadiliko katika nchi yetu.

Naamini ninyi wake za viongozi mmekuwa na mchango mkubwa sana kwa wenza wenu na hii imedhihirishwa na mafanikio yanayoonekana. Lakini, si hilo tu bali akina mama wengi waliokuwa kwenye nafasi na ngazi za maamuzi wameweza kufanya vizuri sana. Hongereni sana. Nawasihi **“Ushirikiano uwe ndio dira katika utendaji wa kazi zenu.”**
Mwanamke akiwezesha anaweza”

Jitahidini kutumia vizuri fursa zinazotolewa na serikali yetu pamoja na mashirika mbalimbali katika kuleta maendeleo yenu zaidi.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 nawaomba tuwaunge mkono wenza wetu wanaogombea pamoja na Wanawake wenzetu wanaogombea nafasi za uongozi.

Mwisho napenda kuwashukuruni tena wote kwa kuwepo hapa leo. Nawatakieni kila la heri na baraka katika shughuli zenu. Tutaendelea kusaidiana katika ujenzi wa taifa letu hili la Tanzania.

WAKINAMAMA TUKIDHAMIRIA TUNaweza! TUSHIRIKIANE KWA PAMOJA KATIKA KULETA MAENDELEO!

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA! MUNGU AWABARIKI!

MUNGU IBARIKI TANZANIA!